TRC Reli na Matukio
Aprili 03, 2019 Toleo Namba 13, Ukurasa namba 1.

# TRC NA WFP WAKUBALIANA KUKARABATI MABEHEWA 40 YA MIZIGO




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe akikata utepe wakati wa hafla ya utiaji saini Makubaliano ya mkataba wa ukarabati wa mabehewa 40 ya mizigo kati ya Shirika la Reli Tanzania – TRC na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani – WFP katika karakana ya reli makao makuu TRC Dar es Salaam hivi karibuni 2019. Picha zaidi Ukurasa 2.

## WAZIRI MKUU MSTAAFU KENYA RAILA ODINGA AMPONGEZA RAIS MAGUFULI KWA UJENZI WA RELI YA KISASA – SGR



Waziri mkuu mstaafu wa Kenya Mhe. Raila Odinga atembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro hivi karibuni 2019.

Mhe. Odinga amefurahishwa na kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wa kujenga reli ya kisasa - SGR ambayo ina umuhimu katika kuchochea maendeleo ya uchumi, viwanda na biashara Tanzania na nchi jirani za Afrika Mashariki.

## TRC NA WFP WAKUBALIANA KUKARABATI MABEHEWA 40 YA MIZIGO




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini Makubaliano ya mkataba wa ukarabati wa mabehewa 40 ya mizigo kati ya Shirika la Reli Tanzania na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani – WFP katika karakana ya reli makao makuu TRC Dar es Salaam hivi karibuni 2019.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kulia) akimuelezea Waziri Mkuu Mstaafu nchini Kenya Mhe. Raila Odinga (wa pili kushoto) kuhusu Maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR alipofanya ziara kuona mradi wa SGR katika eneo la Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019.

Reli na Matukio
Aprili 03, 2019 Toleo Namba 13, Ukurasa namba 3.

## TRC YAENDELEA KUIMARISHA MAWASILIANO KATIKA MAENEO YA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Shirika la Reli Tanzania Mhandisi Felix Mutashobya (kushoto) akikabidhi Vifaa vya Mawasiliano kwa Meneja Msaidizi wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Morogoro – Makutupora Singida Mhandisi Christopher Mang'wela (kulia) katika ofisi ya Makao makuu TRC jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019.

## WAWAKILISHI WA WAJUMBE WA KAMATI YA MADENI YA KITAIFA WAFANYA ZIARA KATIKA MRADI WA SGR




Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu ya Reli kutoka Shirika la Reli Tanzania Mhandisi Felix Nlalio (kulia) akiwaonesha wawakilishi wa wajumbe wa kamati ya Madeni ya Kitaifa mabehewa maalum yanayotumika kumwaga kokoto juu ya reli ya kisasa zilizopo eneo la Soga Kibaha mkoani Pwani hivi karibuni 2019.



Meneja Msaidizi Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Dar – Moro Mhandisi Ayoub Mdachi (kulia) akiwaelezea wawakilishi wa wajumbe wa kamati ya Madeni ya Kitaifa kuhusu stesheni ya reli ya kisasa - SGR inayojengwa eneo la Pugu jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019

Reli na Matukio
Aprili 03, 2019 Toleo Namba 13, Ukurasa namba 4.

# TRC YAANZA UTEKELEZAJI WA MAKUBALIANO YA TRC NA WFP KUKARABATI MABEHEWA 40



Kaimu Mkurugenzi wa Mitambo TRC Mhandisi Lameck Magandi (wa pili kulia) akiwaelezea wajumbe wa kamati ya utekelezaji wa ukarabati wa Mabehewa 40 ya Mizigo kati ya TRC na WFP kuhusu hatua za ukarabati Mabehewa katika karakana ya reli Makao makuu jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2019.

Shirika la Reli Tanzania laanza utekelezaji wa makubaliano yaliyotiliwa saini kati ya Shirika la Reli Tanzania – TRC na Mpango wa Chakula Duniani – WFP kukarabati Mabehewa 40 ya Mizigo ili kuongeza ufanisi katika huduma za usafirishaji wa mizigo hivi karibuni Machi 2019.

Utekelezaji wa makubaliano hayo umeanza kufanyika baada ya kuundwa kamati maalum kwa lengo la kuona namna kazi ya ukarabati itafanyika ikiwemo kujenga karakana mpya katika kiwanda cha Mataruma kilichopo eneo la Pugu jijini Dar es Salaam.

Aidha Shirika linaendelea na Ukarabati wa Mabehewa 200 ya Mizigo kwa awamu ya kwanza kati ya mabehewa 700 yaliyo katika mpango wa ukarabati.



Wajumbe wa kamati maalum ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Shirika la Reli Tanzania - TRC na Mpango wa Chakula Duniani - WFP kukarabati mabehewa 40 ya Mizigo wakikagua behewa ambalo lipo katika hatua za ukarabati katika karakana kuu ya reli Makao makuu TRC jijini Dar es Salam hivi karibuni 2019.

# TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA KWA WANANCHI WALIOPITIWA NA MRADI WA SGR



Afisa wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Bwana Yusuph Mrisho akimhudumia Bwana Fidelis Tairo mmoja wa wananchi wa eneo la Kikongo mkoani Pwani ambao maeneo yao yametwaliwa kupisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR ili aweze kupata Malipo ya fidia ya ardhi hivi karibuni 2019.



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania wakiendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wa Kikongo mkoani Pwani kwa ajili ya kupisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salam - Morogoro hivi karibuni 2019.